# Mwongozo Wa Mwanafunzi

7

## Kanuni za Kikristo

### Zinazohusiana na kanisa la mahali pamoja na kanuni zake



MVMM

Mafunzo ya Vikundi Yanayohusu Maisha Mapya

# Kanuni za Kikristo

## Zinazohusiana na kanisa la mahali pamoja na kanuni zake

Kimeandikwa Na David Batty

Mwongozo Wa Mwanafunzi

Toleo la Tano

MVMM
Mafunzo ya Vikundi Yanayohusu Maisha Mapya

# Kanuni za Kikristo

## Zinazohusiana na kanisa la mahali pamoja na kanuni zake

Kimeandikwa Na David Batty
Mwongozo Wa Mwanafunzi
Toleo la tano

Maandiko yanayotumiwa katika kitabu hiki yametoka kwa:

MAANDIKO: Biblia Takatifu (Union Version). Toleo La 1952, 1974, 1976, 1978. BST, BSK. Yametumiwa Kwa Ruhusa Maalum.

Tafsiri Ya Lugha Rahisi (TLR) itakayofanywa na mtafsiri ili kuleta maana halisi kama inavyosomeka katika lugha ya Kiingereza.

HakiMiliki © 2023, Teen Challenge USA.

Vitabu vya Mwalimu na kila kitu cha mwanafunzi vinavyohusiana na masomo haya ya *Mafunzo ya Vikundi Yanayohusu Maisha Mapya* vinanatawaliwa na Sheria za HakiMiliki. Mpango maalum umefanywa ili kufasiri masomo haya kwa lugha hii yaKiswahili. Masomo haya yanaweza kuchapwa na kugawanywa kwa ajili ya matumizi katika huduma za Teen Challenge na zinazofanana nazo, katika makanisa ya mahali pamoja, shule na mashirika mengine na hata watu binafsi. Pia, yanaweza kupatikana kutoka kwenye mtandao kwenye tovuti hii: www.iTeenChallenge.org Lakini, yasiuzwe. Yatolewe bure. Kwa wanaotaka kuchapisha na kuuza, wapate ruhusa kwa maandishi kutoka Global Teen Challenge.

Kwa mara ya kwanza, somo hili lilichapishwa kwa Kiingereza kwa jina lifuatalo: *Christian Practices, 5th edition*

Somo hili ni sehemu ya mfululizo wa masomo yaitwayo *Mafunzo ya Vikundi Yanayohusu Maisha Mapya* vinanatawaliwa ili kutumiwa makanisani, mashuleni, katika huduma gerezani, huduma za Changamoto Kwa Vijana, na huduma zingine kama hizo zinazofanya kazi na Wakristo Wapya. Vile vile kuna vifaa vingine vinavyopatikana kwa ajili ya mafunzo haya, kama kitabu cha kumwongoza mwalimu, cha kumwongoza mwanafunzi, kitabu cha kuongoza mafunzo cha mwanafunzi, mtihani, na cheti. Ukitaka habari zaidi juu ya masomo haya, wasiliana na:

Global Teen Challenge
PO Box 511
Columbus, GA, 31902 USA
Barua Pepe:gtc@globaltc.org
Tovuti: www.globaltc.org na
www.iTeenChallenge.org

MVMM
Mafunzo ya Vikundi Yanayohusu Maisha Mapya

Mwaka wa Mwisho Kuhakikiwa: 12-2023

# Yaliyomo

**Sura 1. Kanisa La Mahali Pamoja ....................4**
A. Je, Neno "kanisa" linamaanisha nini? ....................4
B. Kwa nini tuna kanisa la mahali pamoja? ....................5
C. Ninawezaje kufurahia kanisa? ....................5
**Sura 2. Jinsi ya kutoa ushuhuda ....................9**
A. Ushuhuda ni nini? ....................9
B. Kwa nini nishuhudie? ....................9
C. Hoja kuu za ushuhuda mzuri ....................9
D. Msaada wa ziada ....................11
E. Kutoa ushuhuda wa maisha yako ....................12
**Sura 3. Jinsi ya kuwa meneja wa Mungu ....................13**
A. Kuwa meneja ni nini? ....................13
B. Je, Mungu amenipa wajibu wa kusimamia nini? ....................13
C. Ni nini humfanya mtu kuwa meneja mzuri wa Mungu? ....................15
D. Ninawezaje kuonyesha kuwa mimi ni meneja wa Mungu? ....................16
E. Mtazamo wangu unaonyesha ikiwa ninafanya kazi kama meneja kwa niaba ya Mungu ....................18
F. Matokeo ya kuwa meneja wa Mungu ....................19
**Sura 4. Ushirika Mtakatifu ....................20**
A. "Je, Ushirika Mtakatifu" inamaanisha nini? ....................20
B. Ni vitu gani maalum vinavyotumika katika ibada ya ushirika mtakatifu? ....................20
C. Kwa nini tunatumia mkate na divai katika ibada ya ushirika mtakatifu? ....................21
D. Je, kusudi la ushirika mtakatatifu ni lipi? ....................21
**Sura 5. Ubatizo wa Maji ....................22**
A. Maana ya kiroho ya ubatizo wa maji ....................22
B. Kwa nini nibatizwe kwa maji? ....................24
C. Ni wakati gani napaswa kubatizwa kwa maji? ....................24
D. Matokeo ya ubatizo wa maji ....................25
**Sura 6. Maombi ....................26**
A. Maombi ni nini? ....................26
B. Je, nitaombaje? ....................27
C. Napaswa kusema nini ninapoomba? ....................27
D. Faida za kuomba ni zipi? ....................29
E. Ninawezaje kupata majibu ya maombi yangu? ....................31
F. Kwa nini sipati majibu ya maombi yangu? ....................31
G. Niombe lini? ....................333
H. Kwa nini maombi ni magumu? ....................34

# Sura ya 1
# Kanisa La Mahali Pamoja

Katika kozi hii, tutazungumzia mada sita tofauti kuhusu kuhusika kwa Mkristo mpya katika kanisa la mahali pamoja. Mada hizi sita ni kanisa la mahali la pamoja, jinsi ya kutoa ushuhuda, jinsi ya kuwa wakili wa Mungu, ushirika, ubatizo kwa maji, na sala. Katika sura hii ya kwanza tutaangalia maswala ya msingi yanayohusiana na kanisa la mahali pamoja na kusudi lake kuwepo kwalo.

## A. Je, Neno "kanisa" linamaanisha nini?

Neno "kanisa" lina maana kadhaa tofauti. Unapozungumza na mtu juu ya kanisa, ni muhimu kujua ni ufafanuzi gani wa neno hili unalomaanisha.

### 1. Ufafanuzi wa kisasa

Hapa kuna fafanuzi chache za neno "kanisa," ambazo zinaonyesha jinsi neno hili linatumiwa kwa leo.

a. Jengo.

b. Kusanyiko, kikundi cha watu wanaoshiriki kwa imani sawa na hukutana pamoja mara kwa mara.

c. Dhehebu – "shirika la kidini linalounganishwa kupitia baraza moja la kisheria na kiutawala katika mkusanyiko wa mahali pamoja" (Kamusi ya Webster). Mifano mingine ni ya Wakatoliki na Walutheri.

d. Wakristo wote duniani.

e. Ibada ya dini.

Katika sura hii tutazingatia majadiliano yetu juu ya kanisa la mahali pamoja, tukimaanisha ufafanuzi b., "Kusanyiko, kikundi cha watu wanaoshiriki kwa imani sawa na hukutana pamoja mara kwa mara."

### 2. "Kanisa" katika Biblia

Katika Biblia, neno "kanisa" kwa kawaida hutumiwa katika mojawapo wa njia hizi mbili:

a. Wakristo wote ulimwenguni.

b. Kusanyiko, kikundi cha watu wanaoshiriki imani sawa na ambao hukutana mara kwa mara.

### 3. Taaswira za kanisa katika Biblia

Biblia hutumia taaswira kadhaa kuonyesha kanisa - haswa katika uhusiano na Kristo.

a. Jengo – Kristo akiwa kama msingi. (1 Wakorintho 3:11; 1 Petro 2:6-8)

b. Mwili – Kristo akiwa kama Kichwa.
(Wakolosai 1:18; Waefeso 1:22-23; Waefeso 5:23-24)

c. Bibi – arusi Kristo akiwa kama mume. (Waefeso 5:25-32)

## B. Kwa nini tuna kanisa la mahali pamoja?

Ni nini kusudi la kanisa la mahali pamoja? Kwa nini kanisa la mahali pamoja lipo? Kuna sababu kuu mbili ni kwa nini tuna kanisa la mahali pamoja.

### 1. Kusaidia Wakristo kukua kwa nguvu kiroho

Sababu kuu ya kuwa na kanisa la mahali pamoja ni kuwasaidia Wakristo kukua wakiwa na nguvu ya kiroho. Kanisa la mahali pamoja lililo na afya litasaidia Wakristo wapya kukuza ukomavu wa kiroho. Ikiwa kanisa la mahali pamoja litashindwa kufanya hivyo, basi litashindwa kutekeleza sababu kuu kuwepo kwalo.

### 2. Kuwaambia kuhusu Kristo wale ambao si Wakristo

Hii ni sababu nyingine muhimu ya kuwa na kanisa la mahali pamoja. Wakati kanisa la mahali linapowasaidia Wakristo kukua wakiwa na nguvu, ndipo Wakristo watawaeleza wengine kuhusu Kristo. (Tazama Matendo 2:42-47.)

## C. Ninawezaje kufurahishwa na kanisa?

Mara nyingi Wakristo wapya huhisi kuwa na wasiwasi kanisani. Labda hawana marafiki wowote wa Kikristo. Au labda mtindo wa ibada ni tofauti. Je, wakristo wapya wanawezaje kujifunza jinsi ya kufurahishwa na kanisa? Je, ni nini kinahitajika ili kuwafanya Wakristo wapya kuhisi kama wao ni washiriki wa kanisa la mahali pamoja?

Hapa kuna miongozo mikuu minne inayofanya kanisa la mahali pamoja kuwa lenye afya. Ikiwa utaanza kufanya mambo haya manne katika kanisa lako, unaweza kufurahishwa na kanisa.

### 1. Tunakusanyika pamoja kwa ushirika *

* Ushirika—kushirikiana, kujadili imani, kukuza urafiki, kuonyesha upendo na kujali wengine.

Moja ya mambo makuu ambayo kanisa la mahali pamoja linapaswa kufanya ni kutoa nafasi kwa watu kujenga urafiki na Wakristo wengine. Ni mahali pa kugundua uzuri wa kupenda na kuwa pamoja na watu. Ushirika huu katika kanisa la mahali pamoja unapaswa kufanya mambo kadhaa:

a. Unatusaidia kujua Wakristo wengine

b. Hutupatia fursa ya kujadili imani zetu

c. Unatuonyesha jinsi ya kujifunza kupenda wengine

d. Unatusaidia kufahamu njia za kusaidiana

e. Hutusaida kuombeana

Wakristo wanahitaji mahali ambapo wanaweza kukutana na kujadiliana kuhusu imani zao.

**Matendo 2:42 Biblia Takatifu (SUV)**

**Nao wakawa wanadumu katika mafundisho ya mitume, katika ushirika, katika kumega mkate na katika kusali.**

Walitumia muda wao kujifunza kutoka kwa mitume, kushiriki katika ushirika mtakatifu, na kushiriki katika chakula cha ushirika na sala.

## 2. Tunakusanyika pamoja kumuabudu* Mungu na kuomba

***** Ibada – kumwambia mtu yeye ni wa maana kwako; kusifu; kupendeza; kuheshimu; kustahi.

Kanisa la mahali pamoja linapaswa pia kuwa mahali ambapo Wakristo wanaweza kujifunza jinsi ya kumwabudu Mungu. Lazima ujifunze kwa uzoefu jinsi ya kumwabudu Mungu. Kwa kuwa ibada inakuwa sehemu ya kawaida ya maisha yako ya kila siku, hii itakuchochea kuwa Mkristo bora kwa kila unachofanya.

Kanisa la mahali pamoja linapaswa pia kuwa mahali ambapo Wakristo hujifunza kumwomba Mungu. Unapojifunza jinsi ya kuomba, utaweza kumleta Mungu maishani mwako. Maombi yako yanahitaji kuwa wazi – jitilie maanani wewe mwenyewe. Jifunze kuomba kwa njia isiyo rasmi. Ongea na Mungu kama vile ungeongea na rafiki yako. Jifunze kuomba kila wakati. Waambie wengine kuhusu mawazo yako kwa Mungu unapoendelea na shughuli zako za kila siku.

## 3. Tunakusanyika pamoja kumsikiliza Mungu

Wakristo wanahitaji kujifunza jinsi ya kumsikiliza Mungu. Kanisa la mahali pamoja linaweza kuwa mahali ambapo Wakristo wanafundishwa jinsi ya kumsikiliza Mungu.

Kuna njia nyingi ambazo Mungu huongea nasi:

a. Kupitia kwa Biblia

b. Kupitia kwa maombi

c. Kupitia kwa karama za Roho Mtakatifu

d. Kupitia kwa Wakristo wengine wacha Mungu

e. Kupitia kwa hali mbalimbali za maisha

Biblia ni mojawapo ya njia kuu ambazo Mungu huzungumza na Wakristo. Ina kila ukweli tunaouhitaji kujua kuhusu kwenda mbinguni na pia jinsi ya kuelewana tukiwa hapa duniani.

Maombi ni njia nyingine kuu ambayo Mungu huwasiliana nasi. Tunapoomba, tunapaswa kuzungumza na kusikiliza. Mungu ataongea nasi ikiwa tutatulia kwa muda na kumpa nafasi ya kumsikiza.

Katika 1 Wakorintho 12:4-11, utapata orodha ya karama tisa za kiroho ambazo Roho Mtakatifu hutoa kwa matumizi ya umma kanisani. Maandiko mengine kadhaa huorodhesha karama zingine ambazo Roho Mtakatifu huwapa Wakristo, kama kuwa mchungaji, mwinjilisti, mwalimu, kusaidia wengine, kutoa, kuongoza wengine (Warumi 12:6-8; Waefeso 4:11-12; 1 Petro 4:7-11).

Karama hizi hutolewa na Roho Mtakatifu ili kutumika kwa huduma. Zawadi hizi hazitolewi ili kuvuta hisia kwa yule aliye na karama hiyo. Mtu halipi kupokea chochote kupokea vipawa hivi, wala sio uthibitisho wa kukomaa kiroho. Roho Mtakatifu hutoa karama hizi kuhudumia kanisa na kwa wasio Wakristo katika jamii.

Njia nyingine ambayo Mungu huongea nasi ni kupitia Wakristo wazee na wenye busara. Mara nyingi, Wakristo waliokomaa wangeweza kutuepusha kutokana na maumivu na mateso mengi ikiwa tungewaendea ili kupata ushauri wao kabla ya kufanya maamuzi makubwa.

Wakati mwingine Mungu hutumia mazingira kusema nasi. Ikiwa hivi karibuni umekuwa Mkristo, Mungu anaweza kukutaka ubadilishe uhusiano wako na marafiki zako wa zamani. Baadhi yao yanaweza kuwa na athari mbaya kwa maisha yako sasa ukiwa Mkristo. Wakati mwingine Mungu anaweka wazi hili unapoomba. Au labda rafiki huyu wa zamani anakukasirikia sana na kusema, “Angalia, unahitaji kufanya uchaguzi. Ikiwa bado unataka kuwa rafiki yangu, basi unahitaji kuachana na habari hizi zote za Yesu ambazo umekuwa ukiongea.”

Mzozo huu unaweza kuwa njia ya Mungu kwako ya kupata umakini ili kuona mabadiliko unayohitaji kufanya kwa marafiki zako.

## 4. Tunakusanyika pamoja ili kusaidiana

Mungu anaahidi kuwatumia Wakristo wanaojitoa kwake. Anaahidi kumpa kila Mkristo uwezo maalum na karama za kutekeleza kazi Yake. Mungu anataka tutumie karama hizi kusaidiana. Karama zingine zinaonekana kuwa zisizo za kawaida, kama uwezo wa kufanya miujiza. Karama zingine zinaonekana asili, kama vile kusaidia wengine. Walakini, karama zote ni za kiungu kwa sababu Mungu ndiye huzipeana.

Kanisa la mahali pamoja linapaswa kuwa mahali ambapo Wakristo wanaweza kujifunza jinsi ya kusaidiana. Inapaswa kuwa mahali ambapo Wakristo wamefundishwa na kuongozwa kuzungumza kuhusu Kristo kwa wengine- watu wote ambao ni Wakristo na wale ambao si Wakristo.

Kwa muhtasari, kanisa la mahali paamoja linapofanya mambo haya manne, unaweza kuwa na hakika kwamba Mungu anafurahishwa, na kwamba kazi ya Mungu itaendelea na kukamilika. Kanisa la mahali pamoja ambalo hufanya mambo haya litakuwa “hai” na la kupendeza. Utafurahiya kuwa sehemu ya kanisa hili. Kanisa ambalo halifanyi mambo haya “litakufa” Watu watachoshwa na kupoteza hamu ya shughuli za kanisa hilo.

Ni muhimu kwako kushiriki katika kanisa la mahali pamoja mara nyingi iwezekanavyo. Unahitaji kukuza urafiki na Wakristo wengine. Unahitaji kufundisha kutoka kwa Neno la Mungu. Unahitaji nafasi ya kuwapa wengine kile ambacho Mungu amekupa.
Unahitaji kushiriki kwa kazi ya Mungu.

# Sura ya 2
# Jinsi ya kutoa ushuhuda

## A. Ushuhuda ni nini?

Ushuhuda ni ukweli wa kibinafsi unaosemwa na shahidi. Katika sura hii, tutajadili jinsi ya kutoa ushuhuda kama inavyohusiana na kuwa Mkristo. Katika muktadha huu, ushuhuda ni “kuwaeleza wengine kile Kristo amefanya na bado anafanya katika maisha yako.”

## B. Kwa nini nitoe ushuhuda?

Ikiwa Mungu amekusaidia na anabadilisha maisha yako, unahitaji kuwaambia wengine kumhusu. Kutoa ushuhuda inaweza ukuwa siyo rasmi kama vile kuzungumza na mtu wa familia kile Mungu anafanya katika maisha yako. Unaweza kuwa na nafasi ya kuutoa ushuhuda wako kwa njia rasmi zaidi — labda katika mkutano wa kanisa au wa shule. Hapa kuna sababu kadhaa kwa nini unapaswa kutoa ushuhuda wako kwa wengine:

1. Ni njia ya kumtii Kristo. (Mathayo 28:19-20).
2. Kunanipa nafasi ya kuimarisha imani na tumaini langu kwa Mungu. Kunanisaidia kuwa Mkristo aliyeimarika zaidi.
3. Kunanipa nafasi ya kuchukua msimamo ulio wazi kwa Mungu (Matendo 5:29)
4. Kunanipa nafasi ya kuwasaidia wengine. Kunaweza kusaidia wengine kumhusisha Mungu na maisha yao.
5. Kunanipa nafasi ya kuleta utukufu kwa Mungu, kwa hivyo Yeye hupata sifa kwa mabadiliko yanayoonekana maishani mwangu.
6. Kunanipa fursa ya kumshinda Shetani. (Ufunuo 12:11)

## C. Hoja kuu za ushuhuda mzuri

Kwenye ukurasa wa 12 wa mwongozo huu, maelezo ya ziada yametolewa juu ya kile cha kujumuisha wakati una nafasi ya kutoa ushuhuda wa maisha yako. Wakati unapotoa ushuhuda wako wa maisha kwa mtu mwingine, mara nyingi utajumuisha maelezo ya maisha yako ya zamani katika dhambi.

Tafadhali elewa kuwa, kinachofuata katika sehemu hii ni kuzungumzia fursa zingine nyingi utakazokuwa nazo kuzungumza na watu kile Mungu anafanya katika maisha yako.

Kila ushuhuda unaotoa hauitaji kujumuisha maelezo ya maisha yako ya zamani katika dhambi. Unahitaji kuweka mwelekeo wako kwa kunena yale ambayo Mungu amefanya katika maisha yako, si yale ambayo shetani alifanya hapo zamani.

Unapokuwa na nafasi ya kutoa ushuhuda wako kwa wengine, hapa kuna mambo manne ambayo unaweza kutaja katika ushuhuda wako.

## Sehemu 4 Kuu za Ushuhuda Mzuri

1. Eleza eneo moja katika maisha yako ya kila siku pale ambapo Mungu anakusaidia kukua.
2. Taja mstari mmoja katika Biblia ambao umekusaidia kukua katika eneo hili la maisha yako. Ikiwa umekariri aya hiyo, basi inukuu. Au soma kutoka kwa Biblia yako.
3. Eleza jinsi umeutumia mstari huu kukusaidia katika eneo hili moja la maisha yako. Usihubiri. Eleza kwa njia rahisi na inayofaa jinsi aya hii inakusaidia. Eleza jinsi aya hii inahusiana na eneo la maisha yako ambapo Mungu anakusaidia kukua.
4. Toa mfano mmoja maalum kutoka siku chache zilizopita kuonyesha jinsi ulivyotumia aya hii. Mpe Mungu sifa kwa kukusaidia kukua.

Wakati mwingine ni vigumu kupata maoni mapya ya kutumia katika ushuhuda. Chati ifuatayo inaweza kukusaidia kwa hili.

### Mfano wa Kujifunza wa Maisha-kwa-Maisha

**1. Orodhesha hali zinazokufadhaisha**
Orodhesha hali ambazo huwa rahisi kunighadhabisha, kunifadhaisha, kunikasirisha kunikatisha tamaa, au wakati ninahisi kuwa chini kutokana na shinikizo.

**2. Muulize Mungu swali hili:**
"Mungu, unajaribu kunifundisha nifanye nini leo?" Jaribu kuiangalia hali hii kwa mtazamo wa Mungu.

3. **Tafuta eneo moja katika maisha yangu ya kila siku ambapo ninataka kukua**
Angalia baadhi ya mambo uliyoorodhesha katika hatua # 1. Ikiwa una wakati mgumu wa kufikiria kuhusu sehemu amabozo unatakiwa kuzifanyia kazi, angalia orodha ya vitu vilivyo kwenye 1 Wakorintho 13:4-8.

**4. Husisha hili na masomo yangu ya Biblia**
Je, Biblia inasema nini kuhusu eneo hili la maisha yangu ambalo ninataka kukua?

**5. Weka orodha ya vitu ambavyo ninaweza kukamilisha leo**
Weka malengo. Tengeneza orodha ya mambo unayoweza kufanya ili utekeleze kibinafsi kile ambacho kifungu cha maaandiko kinakuambia ufanye. Chagua lengo moja na ulifanye leo.

**6. Tathmini matokeo**
Baadaye siku hiyo hiyo au siku inayofuata, kagua kile kilichotokea wakati ulijaribu kufikia lengo ulilolweka. Eleza hali hiyo na ueleze jinsi lengo lako lilikusaidia (au halikukusaidia) kutumia aya hii kwa maisha yako.

# D. Msaada wa ziada

## 1. Ushuhuda wako uwe mfupi, chini ya dakika tano

Wengine huona ni rahisi kusimama mbele ya watu na kutoa ushuhuda. Baada ya yote, unazungumza juu yako mwenyewe, na kile Mungu amefanya katika maisha yako! Pamoja na kwamba hili linapendeza kwako, wale ambao wanasikiliza wanaweza kuchoka ikiwa ushuhuda wako ni mrefu sana, kwa hivyo uwe mfupi chini ya dakika tano. Panga kugawanya wakati huu kwa usawa katika sehemu nne za ushuhuda wako (kama ilivyoelezewa chini ya Hoja ya C kwenye ukurasa wa 9-10 wa Mwongozo wa Wanafunzi).

## 2. Panga kile utakachosema katika ushuhuda wako

Watu wengine husema, “Sitapanga chochote. Kwa njia hiyo nitakaposimama Roho Mtakatifu ataweka maneno kinywani mwangu.” Kuna njia bora ya kutoa ushuhuda wako. Acha Roho Mtakatifu akusaidie unapopanga ushuhuda wako.

Unaweza kuandika maelezo machache juu ya kile unachopanga kusema. Ikiwa haujawahi kutoa ushuhuda hapo awali, unaweza kutaka kuandika ushuhuda wako. Hili litakusaidia kupata mazoezi ya kuweka pamoja sehemu zote nne za ushuhuda wako.

## 3. Hakikisha ushuhuda wako wote unaleta utukufu kwa Mungu

Iweke wazi kuwa Mungu amekubadilisha kupitia nguvu zake. Usifanye ionekane kana kwamba ulifanya haya yote wewe mwenyewe. Yesu alisema, “Bila mimi huwezi kufanya chochote.” Kumbuka hilo. Unapotoa ushuhuda, usilete utukufu kwako wala usitukuze dhambi.

## 4. Omba Roho Mtakatifu akusaidie kusema mambo yanayofaa

Sababu moja ni kwa nini tunatoa ushuhuda wetu ni kusaidia watu wengine. Hata hivyo, hatuwezi kumsaidia mtu mwingine yeyote kwa “kufanya mambo yetu wenyewe tu.” Ni pale tu Roho Mtakatifu atatumia kile unachosema ndipo ushuhuda wako unaweza kuwa na thamani ya kweli. Kuwa mwangalifu kwa Roho Mtakatifu. Omba na umwombe akuongoze katika kusema kile Anachotaka useme.

# E. Kutoa ushuhuda wa maisha yako

Unaweza kuwa na nafasi ya kuwaambia wengine juu ya maisha yako ya zamani na jinsi ulivyokuwa Mkristo. Mara nyingi Mungu hutumia aina hii ya ushuhuda kusaidia watu kuona thamani ya kuwa Mkristo.

Aina hii ya ushuhuda inaweza kutumiwa vibaya, pia. Wakati mwingine watu huanza kujisifu juu yao wenyewe. Matokeo yake wanajiletea utukufu, lakini sio kwa Mungu.

Unapokuwa na nafasi ya kutoa ushuhuda wako wa maisha yako kwa wengine, hapa kuna mambo manne ambayo unaweza kuzungumzia:

## 1. Eleza matokeo ya dhambi

Toa mfano *mmoja* tu kutoka kwa maisha yako ya zamani kuonyesha matokeo ya dhambi. Sema ni kwa nini ulikuwa na shida (ni nini kilisababisha shida). Kuwa wazi (kwa uhakika), lakini usijisifu juu ya dhambi hiyo.

Usifanye uzoefu wako wa zamani kuonekane kama ulikuwa wa kufurahisha kuliko kuwa Mkristo. Eleza jinsi dhambi ilivyoharibu maisha yako na kukuzuia kupata furaha ya kweli na amani. Usitumie wakati wako wote katika sehemu hii. Hakikisha unatumia wakati sawa kwa sehemu zingine tatu za ushuhuda wako.

## 2. Eleza jinsi ulivyofikia hapa na jinsi ulivyokuwa Mkristo

Viseme vitu hivyo ambavyo vilikusaidia kufanya uamuzi wa kuwa Mkristo. Hakikisha kwamba msikizaji wako anaelewa kwamba Kristo alikuokoa.

## 3. Eleza jinsi maisha yako yalivyobadilika tokea ulipokuwa Mkristo

Usiseme, “Mungu amenisaidia kushinda shida zote.” Toa mfano wa jambo moja ambalo Mungu amekusaidia nalo tokea ulipokuwa Mkristo. Unaweza kuzungumzia mstari wa Bibilia ambao umekusaidia. Hata hivyo, usijaribu kuhubiri ujumbe mfupi katika ushuhuda wako. Wacha mhubiri ahubiri. Jukumu lako ni kutoa tu ushuhuda mfupi wa maisha yako.

## 4. Waambie mipango na malengo ya maisha yako ya siku za zijazo

Unaweza kuhitimisha ushuhuda wako kwa kunenea mipango na malengo yako. Waulize wakuombea. Waambie unataka kujua mapenzi ya Mungu maishani mwako, na kufanya kile anachotaka ufanye. Sehemu hii ya ushuhuda wako inaweza kuwa fupi mno.

# Sura ya 3
# Jinsi ya kuwa meneja wa Mungu

Unapokuwa Mkristo, wewe huanza uhusiano mpya na Mungu. Unakuwa mwana wa Mungu (Yohana 1:12). Mungu huja na kuishi ndani yako (Yohana 14:17, 23). Tunakuwa marafiki na Mungu. Tunajifunza jinsi ya kuhisi na kupokea upendo Wake. Muda si muda, tunajifunza jinsi ya kuonyesha upendo wetu kwake. Sisi huanza kuona kwamba Mungu hujibu maombi yetu.

Mabadiliko mengine muhimu ambayo yanahitaji kufanyika maishani mwetu yanahusiana na Biblia. Tunahitaji kujifunza Biblia kila siku, na kutafuta kile Mungu anasema juu ya shida na changamoto tunazokabiliana nazo maishani mwetu. Tunahitaji kuanza kutumia majibu haya mapya katika maisha yetu ya kila siku. Tunahitaji kujibu kwa njia ambayo Mungu anataka tujibu.

Je, ni nini Mungu amekufanya kuwa msimamizi wake leo? Sehemu moja kuu ya uhusiano wetu na Mungu inahuisha vitu ambavyo ametupatia. Majukumu fulani huja pamoja na vitu vyote vizuri ambavyo Mungu anatupatia. Tunaweza kusema kwamba sisi sote ni mameneja wa Mungu. Ametupatia vitu vingi. Sasa tuna jukumu la kufanya kazi nzuri ya kusimamia vitu hivi. Tunapaswa kujifunza kutumia karama zake kwa busara.

## A. Meneja ni nini?

Kwa hivyo meneja ni nini?

1. Meneja ni mtu aliyeajiriwa kutunza mali ya mtu mwingine au pesa.
2. Meneja sio mmiliki. Meneja humfanyia kazi mmiliki.
3. Kila Mkristo ni meneja wa Mungu. Kuwa Mkristo inamaanisha kuwa Mungu ndiye Kiongozi wa maisha yangu. Yeye ndiye mmiliki wangu, lakini mimi sio tu bandia au roboti. Anatarajia nifanye kazi kama Mkristo katika jamii.

Kuwa msimamizi wa Mungu si kitu maalum kwa Wakristo wachache tu. Mungu anatarajia watoto wake wote kuwa mameneja wazuri.

## B. Je, Mungu amenipa wajibu wa kusimamia nini?

### 1. Wakati

Ikiwa ungepewa milioni 86,400 na ikubidi utumie leo, ungeitumiaje? Tuseme ulipewa kiasi hiki kila siku na sharti ulilazimika kurudisha chochote ambacho haukutumia siku hiyo. Unafikiri unaweza kufanya kazi nzuri kiasi gani, kusimamia pesa nyingi kila siku?

Mungu amekupa sekunde 86,400 za kutumia kila siku. Wakati wako ni moja wapo ya mambo makuu ambayo Mungu amekupa. Je, unausimamia vizuri wakati wako?

## 2. Pesa

Wengi wetu hatuna shilingi milioni 86,400 ya kutumia kila siku. Lakini hata ikiwa ni shilingi chache tu, tuna jukumu la kuzisimamia kwa njia inayompendeza Mungu.
“Je, Lazima nitoe pesa zangu zote kwa Mungu?” Hapana, lakini 2 Wakorintho 9:7 inatupatia ushauri mzuri kuhusu jinsi ya kutumia pesa zetu.

**2 Wakorintho 9:7 Biblia Takatifu (SUV)**

**Kila mtu atoe kama anavyokusudia moyoni mwake, si kwa uchoyo au kwa kulazimishwa, kwa maana Mungu humpenda yeye atoaye kwa moyo mkunjufu.**

Wengi wetu labda tungependa kuwa na pesa nyingi kuliko zile tulizo nazo leo. Lakini Mungu anataka tudhibitishe jinsi tunavyoweza kusimamia kile tulicho nacho tayari. Ikiwa tutathibitisha kuwa tunaweza kusimamia kiasi kidogo vizuri, basi anaweza kutupatia kiasi kikubwa cha kusimamia.

## 3. Karama za Roho Mtakatifu

Roho Mtakatifu ana karama nyingi ambazo anataka kuwapa watoto wake. Yeye ni mwangalifu kuhusu kuzitoa karama hizi kwa Wakristo. Tunahitaji kutumia kwa uangalifu karama Zake. Maandiko kadhaa huorodhesha baadhi ya karama hizi: 1 Wakorintho 12, Warumi 12, 1 Petro 4, na Waefeso 4.

## 4. Jamii na mahusiano

Kuwa meneja wa Mungu kunahusiana aje na jamii- hasa ikiwa siishi na wao? Tuna fursa za kusimamia mahusiano yetu na watu hawa. Mungu hutupatia majukumu kadhaa ambayo huhusisha mahusiano ya kijamii.

## 5. Kazi

Kazi yako — unaipenda au unaichukia? Je, unafurahiya kufanya kazi? Je, ungepimaje mtazamo wako juu ya kazi yako? Hili ni eneo lingine muhimu la shughuli zetu za kila siku ambapo tunaweza kuonyesha jinsi tulivyo mameneja wa Mungu.

**Wakolosai 3:23-24 Biblia Takatifu (SUV)**

**Lolote mfanyalo, fanyeni kwa moyo kama watu wanaomtumikia Bwana, na si wanadamu, 24 kwa kuwa mnajua kwamba mtapokea urithi wenu kutoka kwa Bwana ukiwa thawabu yenu. Ni Bwana Yesu Kristo mnayemtumikia.**

# C. Ni nini humfanya mtu kuwa meneja mzuri wa Mungu?

## 1. Ukuaji uliosawazishwa

Ukuaji uliosawazishwa ni moja wapo ya sifa kuu za meneja mzuri. Mungu anataka kuona ukuaji wa kibinafsi katika maisha yako. Anataka pia kuona ukuaji katika kazi yako na wengine. Tunahitaji kufikia na kusaidia watu wengine. Kuna fursa nyingi za utumishi wa Kikristo, lakini kuwa na usawazisha ndio ufunguo.

## 2. Meneja mzuri hujifunza (kukasimu) kukabidhi majukumu

Wasimamizi wazuri hawajaribu kufanya kila kitu peke yao. Wano hujifunza jinsi ya kupeana majukumu na kufanya kazi na watu wengine. Mungu anataka Wakristo wapya kushiriki kikamilifu katika kanisa la mahali pamoja. Tunahitaji kujifunza jinsi ya kuishi na Wakristo wengine.

## 3. Mmiliki wangu ni nani – Je, kiongozi wangu ni nani? Ni Mungu!

Ikiwa unataka kuwa msimamizi bora, mjue Mungu vyema, Anakupenda na anataka kukuza urafiki wa karibu na wewe. Ukiwa karibu na Mungu, ndivyo ilivyo rahisi kujua anachotaka ufanye.

## 4. Upendo ni sehemu kubwa sana ya kuwa meneja mzuri zaidi wa Mungu

Wasimamizi ambao wanaonyesha upendo kwa wengine ni watu wazuri kufanya kazi nao. Wakolosai sura ya 3 inatoa orodha kamili ya vitu ambavyo vinaweza kukusaidia kuwa msimamizi mwema.

**Wakolosai 3:14 Biblia Takatifu (SUV)**

**Zaidi ya maadili haya yote jivikeni upendo, ambao ndio unaofunga kila kitu pamoja katika umoja mkamilifu.**

## 5. Uaminifu

Alama nyingine ya meneja bora ni uaminifu. Kuwa mwaminifu inamaanisha kuwa mtu thabiti na mwaminifu.

**1 Wakorintho 4:2 Biblia Takatifu (SUV)**

**Tena, litakiwalo ni mawakili waonekane kuwa waaminifu.**

Wakati mwingi, njia rahisi ya kuondokea hali fulani ni kukata tamaa. Lakini mameneja wazuri ni waaminifu. Wanaweza kutegemewa. Wanakamilisha kazi waliyopewa na Mungu kufanya.

**2 Wakorintho 8:11**

**Sasa ikamilisheni kazi hii kwa shauku kama mlivyoanza, jitoleeni kulingana na uwezo wenu.**

### 6. Utiifu

Utiifu ni mtindo wa maisha ambao unaashiria kuwa mtu ni mmeneja mzuri wa Mungu. Utii unahusu sheria za Mungu na sheria za mwanadamu.

## D. Ninawezaje kuonyesha kuwa mimi ni meneja wa Mungu?

### 1. Wakati wangu

a. Fanya Jumapili kuwa siku maalum. Toa siku moja kwa wiki kumwabudu Mungu na kushirikiana na Wakristo wengine katika kanisa lako (Kutoka 20:8-10).

b. Kuwa na ibada za kibinafsi kila siku. Chukua muda kusoma Biblia na kuomba.

c. Toa wakati wako kwa ajili ya Kikristo. Mathayo 25:31-46 huorodhesha njia kadhaa ambazo unaweza kuhusika kwa kazi ya Kikristo.

d. Chukua muda wa kuwahubiria wengine. Waambie kuhusu maisha mapya uliyonayo.

### 2. Kazi yangu

#### a. Fanya kazi ili kujikimu na kukimu familia yako

Biblia inatoa maagizo maalum kwa waume na kina baba kuhusu majukumu yao katika eneo hili.

**1 Timotheo 5:8**

**Kama mtu hawatunzi wale wa jamaa yake, hasa wale wa nyumbani mwake mwenyewe, ameikana imani, tena ni mbaya kuliko yeye asiyeamini.**

Mungu anaeleza kauli iliyo wazi kuhusu majukumu ya baba au mume. Hata kama haujawahi kuoa mama wa watoto wako, Mungu anasema bado una jukumu la kuwatunza watoto hao. Vivyo hivyo ni kweli ikiwa umempa talaka mke wako — bado una jukumu la kumtunza yeye na watoto wako.

Mungu hana mpango wa kuwasaidia watu ili Wakristo waweze kukaa tu kitako na kutofanya chochote huku Mungu akituma pesa. Mungu hafanyi kazi kwa njia hiyo. Anatarajia tufanye kazi kwa bidii wakati tunapofanya kazi.

| | |
|---|---|
| Wakolosai 3:23 2 | 1 Wathesalonike 4:11 |
| 2 Wathesalonike 3:10 | 2 Wakorintho 8:11 Biblia Takatifu (SUV) |

### b. Fanya kazi nyumbani

Mungu anatarajia utunze nyumba yako, makazi yako na chumba chako. Ikiwa umeoa, na wewe ni mume, una jukumu la kuwa kiongozi nyumbani. Usitarajie mke wako kufanya kazi zote za nyumbani. Kuwa tayari kumsaidia na kushiriki katika kusaidia kwa kila njia uwezavyo. Ni muhimu kwamba watoto wako wakuone unafanya kazi. Wao hujifunza kwa kuona mfano. Hakikisha watoto wako wana mfano mzuri wa kufuata.

## 3. Mali zangu (pesa na vitu nilivyo navyo)

### a. Mtolee Mungu

Mtolee Mungu ili uhusike katika kusaidia kujenga kazi yake hapa duniani. Usijaribu kujenga “Ikulu” yako mwenyewe. Toa kwa ajili ya kazi ya Mungu na umtazame akikubariki. Wakristo wengi hutoa angalau moja ya kumi ya kile wanachopata kwa Mungu. Hili linaitwa fungu la 10 ya kile unachopata. Tazama Malaki 3:7-10.

### b. Watolee wengine walio na mahitaji

Tunapaswa kuwatolea wengine kwa sababu tunapenda kutoa, si kwa sababu tunalazimishwa kutoa.

| | |
|---|---|
| Luka 6:38 | Wagalatia 6:7-10 |
| 2 Wakorintho 8:9 | 1 Yohana 3:17-18 |

### c. Mpe Mungu umiliki wa kila kitu chochote kingine

Vitu vyote ulivyo navyo umepewa na Mungu. Fanya uamuzi wa kumpa Mungu haki za umiliki wa pesa na mali zako zote.

Mungu amempa kila mmoja wetu uwezo tofauti. Sisi sote tuna jukumu la kufanya kazi nzuri ya kukuza na kutumia uwezo huu.

# E. Mtazamo wangu unaonyesha ikiwa ninafanya kazi kama meneja kwa niaba ya Mungu

Matendo yangu peke yake hayathibitishi kuwa ninafanya kazi kama meneja wa Mungu. Huwa ni zaidi ya vitendo vya nje. Motisha wangu uko katika kusudi la kuwa meneja wa Mungu.

## 1. Je, upendo ni motisha wako?

Mungu anataka umtumikie kwa sababu unampenda. Mungu anaweza kuona ikiwa upendo ndio sababu yako ya kufanya haya yote. Upendo hutoa sababu thabiti ni kwa nini ninataka kuwa msimamizi mzuri wa Mungu.

## 2. Je, unataka kuwa meneja wa Mungu?

**2 Wakorintho 9:7**

**Kila mtu atoe kama anavyokusudia moyoni mwake, si kwa uchoyo au kwa kulazimishwa, kwa maana Mungu humpenda yeye atoaye kwa moyo mkunjufu.**

Ikiwa utachagua kuwa msimamizi wa Mungu, fanya hivyo kwa sababu unataka. Mungu hatakulazimisha kufanya chochote. Haifanyi kazi kwa njia hiyo. Mungu hakutazami wewe kama mtumwa wake. Anakuona kama mtoto Wake. Lakini Mungu pia anawatendea watoto wake kama watu wazima. Anatupatia uhuru mwingi, lakini pamoja na haya huja na majukumu.

## 3. Je, ni nini kuhusu sheria za Mungu?

Wakristo wengine wana sheria zinazopita mipaka katika uhusiano wao na Mungu. Kile wanachoangalia ni sheria zilizo katika Biblia. Wanafikiri kuwa Mkristo kunamaanisha kutii sheria hizi zote. Wanasema, “Kanuni namba 367 inasema lazima niwe msimamizi wa Mungu, kwa hivyo nadhani itabidi nifanye hivyo, pia.”

Mungu anataka umtumikie kwa sababu unampenda na unataka kuwa mtoto wake.

Biblia inatoa maagizo wazi kuhusu maana ya dhambi. Tunahitaji kujitolea kumtii Mungu kila siku. Kufanya uchaguzi ulio sahihi si rahisi kila wakati, na mara nyingi tunashindwa. Mungu bado anatupenda, na yuko tayari kutusamehe na kutusaidia kukua na nguvu zaidi dhidi ya changamoto inayofuata ambayo tutakabiliana nayo.

Somo la kumtii Mungu linafunzwa kwa undani zaidi katika kozi ya *Mafunzo ya Vikundi kwa Maisha Mapya* iitwaya **Utiifu kwa Mungu**.

# F. Matokeo ya kuwa meneja wa Mungu

Hapa kuna matokeo kadhaa ya kuwa meneja mzuri wa Mungu:

1. Mungu atakupa yote *unayohitaji* (sio mambo yote unayotaka).

   Luka 6:38

   2 Wakorintho 9:8

   Wafilipi 4:19

2. Mungu atakupa uzima wa milele.

   Mathayo 25:31-46

3. Mungu atakupa majukumu zaidi.

   Luka 16:10

# Sura ya 4
# Ushirika Mtakatifu

## A. “Je, Ushirika Mtakatifu” unamaanisha nini?

Makanisa mengi hufanya “ushirika mtakatifu” kuwa sehemu ya kawaida ya huduma zao za kanisa. Sehemu hii ya huduma ya kanisa hubeba maana ya kipekee sana, inayohusiana na kifo cha Yesu. Lakini neno “ushirika Mtakatifu” lina maana zaidi ya moja — zote zina maana maalum kwa Wakristo.

1. Kushiriki
2. Ibada maalum katika makanisa

Ibada hii maalum ya kanisa imepewa majina tofauti. Hapa kuna baadhi yao:

a. Ushirika Mtakatifu

b. Ekaristi (Hili ni neno la Kiyunani linalomaanisha, “kutoa shukrani.”)

c. Meza ya Bwana

d. Ibada ya ushirika wa Bwana

Katika sura hii, tutazingatia huduma hii ya ushirika inayotumiwa makanisani leo. Katika 1 Wakorintho 11:23-34, Paulo anaelezea kwa kina maana na kusudi la huduma ya ushirika.

## B. Ni vitu gani maalum vinavyotumika katika ibada ya ushirika mtakatifu?

1. Mkate (1 Wakorintho 11:23-24)

   Mkate unawakilisha mwili wa Yesu. Mwili wake ulipigwa na kuchubuliwa ili tuweze kuponywa (Tazama Isaya 53:5).

2. Mvinyo au sharubati ya zabibu (1 Wakorintho 11:25)

   Mvinyo au sharubati ya zabibu inawakilisha damu ya Yesu. Alitoa maisha yake ili tuweze kuokolewa kutoka kwa adhabu ya dhambi. Makanisa mengi hutumia sharubati ya zabibu, ili wale watu wanaopambana na ulevi wasijaribiwe kuanza kunywa tena.

## C. Kwa nini tunatumia mkate na divai katika ibada ya ushirika mtakatifu?

1. Kusaidia kufanya kifo cha Yesu kiwe halisi zaidi kwetu.
2. Mkate na divai ni mafunzo kwetu. Unaiona, unahisi, unanusa, na unaonja. Vitu hivi vinaweza kutusaidia kuibua au kuona katika akili zetu ukweli wa kifo cha Yesu.

## D. Je, kusudi la ushirika mtakatatifu ni nini?

1. Kumwabudu Mungu. (1 Wakorintho 11:24-26)
2. Kukumbuka kuwa Yesu alikufa kwa ajili yetu. (1 Wakorintho 11:24-25)
3. Kutukumbusha kutarajia kuja kwa Yesu tena. (1 Wakorintho 11:26)
4. Kutupatia fursa ya kujichunguza moyoni (kuchunguza maisha yetu). (1 Wakorintho 11:27-32)
   a. Tunaweza kuungama dhambi zetu kwa Mungu.
   b. Tunaweza kuona ikiwa tumefikia malengo yetu.
5. Kutusaidia kutazama uhusiano wetu na wengine. (1 Wakorintho 11:29)
   a. Tunaweza kuomba msamaha ikiwa tumemkosea au kumuumiza mtu.
   b. Tunaweza kumtia mtu moyo.
   c. Tunaweza kuwashukuru wengine kwa kitu ambacho wamefanya.

"Mwili wa Bwana" (katika 1 Wakorintho 11:29) inazungumzia kuhusu Wakristo wengine walio katika kanisa lako. Haizungumzii juu ya mwili wa Yesu wakati alikuwa hapa duniani. Tazama pia 1 Wakorintho 12:12-31.

# Sura ya 5
# Ubatizo wa Maji

Kusudi letu katika sura hii ni kuelezea maana ya kiroho ya ubatizo wa maji na ni kwa nini ni muhimu kwa Wakristo wapya. Ubatizo wa maji haumfanyi mtu kuwa Mkristo.

Ubatizo wa maji ni ishara au thibitisho la kuonyesha kuwa mabadiliko ya kiroho yamefanyika katika maisha yangu. Ninauambia ulimwengu kuwa nimekuwa Mkristo.

## A. Maana ya kiroho ya ubatizo wa maji

Katika Warumi 6:1-10 na Wagalatia 2:20 Paulo anajadili maana ya kiroho ya ubatizo wa maji.

### 1. Ninajitambulisha na Kristo katika kusulubiwa kwake

**Wagalatia 2:20**

**Nimesulubiwa pamoja na Kristo na siishi tena, lakini Kristo anaishi ndani yangu. Maisha ninayoishi mwilini, ninaishi kwa imani katika Mwana wa Mungu, ambaye alinipenda na akajitoa mwenyewe kwa ajili yangu.**

**Warumi 6:6 Biblia Takatifu (SUV)**

**Kwa maana twajua kwamba utu wetu wa kale ulisulubiwa pamoja naye ili ule mwili wa dhambi upate kuangamizwa, nasi tusiendelee kuwa tena watumwa wa dhambi.**

Utu wangu wa kale wa dhambi umesulubiwa pamoja na Kristo. Huu pia ni wakati wangu wa kutoa taarifa hadharani kwamba ninaweka tabia zangu za dhambi na mitazamo yangu ya dhambi msalabani. Ninachagua kuziacha msalabani, na kukabiliana na maisha mapya ambayo Kristo amenipa bila kuwepo na tabia na mitazamo hii ya kale. Ninatambua lazima nizifanye njia hizi za zamani zife ikiwa nitapokea uhuru wa kweli katika Kristo. Natambua pia kuwa huu unaweza kuwa mchakato wa kuumiza, lakini si kwa uchungu kama alioupitia Kristo pale msalabani.

### 2. Ninajitambulisha na Kristo katika kifo chake

**Warumi 6:3 Biblia Takatifu (SUV)**

**Au hamjui ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika mauti yake?**

Ubatizo wa maji ni tamko kwa umma kwamba nimekufa kwa ajili ya asili yangu ya kale ya dhambi maishani. Inaweza kuwa rahisi kusema hivi, lakini maisha halisi ya kila siku kutoka kwa tamko hili yanaweza kuwa changamoto ngumu. Kifo maana yake ni kujitenga.

Ninahitaji kuona jinsi nilivyokuwa ninaishi hapo kale jinsi ya kihalisia - njia ya uharibifu wa milele. Lakini Kristo ameingilia kati na kuniokoa. Ninachagua kufa kwa njia ya zamani ya kuishi, na kuchagua kuishi katika maisha mapya ambayo Kristo huleta kwangu. Ninapokuwa ninapatizwa kwa maji ninasema kwamba, -sehemu yangu moja imekufa — sehemu yangu ya dhambi yenye ubinafsi.

Ishara hii ya kifo haimaanishi kuwa nitakuwa huru kutoka kwa majaribu. Kinyume kabisa cha hili ni kweli. Majaribu ya kurudia njia hiyo ya maisha ya zamani yatakuja. Lakini lazima nikumbuke kwamba nimeyazika kaburini maisha hayo ya zamani. Kwa nini niyachimbue maisha ya zamani yanukayo, yaliyooza, yaliyozeeka na yaliyokufa?

## 3. Ninajitambulisha na Kristo katika kuzikwa kwake

**Warumi 6:4 Bibilia Takatifu (SUV)**

**Kwa hiyo tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti, ili kama vile Kristo alivyofufuliwa kutoka kwa wafu kwa utukufu wa Baba, vivyo hivyo sisi nasi pia tupate kuenenda katika upya wa uzima.**

Baada ya Kristo kufa, aliondolewa msalabani na kuzikwa kaburini. Wakati ninabatizwa kwa maji, ninatoa taarifa kwamba nimezika maisha yangu ya zamani ya dhambi-njia ile ya zamani ya kuishi. Kwa kweli, Kristo ameifanya kazi hiyo. Ninachohitaji kufanya ni kukubali njia Yake. Njia yangu ya zamani ya kuishi ilikuwa inanielekeza kwa uharibifu. Nilipokubali kuwa Mkristo, kwa hiari niliacha njia yangu ya zamani ya kuishi, nikaipigilia msalabani, na nikaihesabu kuwa imekufa.

Kilicho kufa kimezikwa. Wakati ninazama ndani ya maji wakati wa ubatizo, ni ishara ya kuzikwa.

## 4. Ninajitambulisha na Kristo katika ufufuo wake

**Warumi 6:4-5**

**Kwa hiyo tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti, ili kama vile Kristo alivyofufuliwa kutoka kwa wafu kwa utukufu wa Baba, vivyo hivyo sisi nasi pia tupate kuenenda katika upya wa uzima. 5 Kwa maana ikiwa tumeungana naye katika mauti yake, bila shaka tutaungana naye katika ufufuo wake.**

Ubatizo wa maji ni ishara kwamba nimepewa maisha mapya. Nimezaliwa mara ya pili. (Yohana 3:3, 7) Kuzaliwa kiroho — wokovu — sio ndoto tu akilini mwangu, ni ukweli thabiti. Kama vile Kristo alifufuliwa kutoka kwa wafu, vivyo hivyo kuibuka kwangu kutoka kwa maji ni ishara ya maisha mapya ambayo Mungu amenipa.

Wakati nilikuwa nikiishi katika njia zangu za zamani za dhambi, nilikuwa nimekufa kiroho. Kwa sababu Kristo anaishi ndani yangu sasa, mimi ni hai kweli kweli — nina maisha mapya ndani yangu.

Sasa kwa kuwa nimepewa maisha mapya, sihitaji kuogopa kifo ambacho kiliningojea kwa sababu ya maisha yangu ya zamani. Niko hai kwa sababu Kristo anaishi ndani yangu.

### 5. Ninajitambulisha na Kristo katika njia yake mpya ya kuishi

**Wagalatia 2:20**

**Nimesulubiwa pamoja na Kristo, wala si mimi tena ninayeishi, bali Kristo ndiye aishiye ndani yangu. Uhai nilio nao sasa katika mwili, ninaishi kwa imani ya Mwana wa Mungu, aliyenipenda na kujitoa kwa ajili yangu.**

Ninapochagua kubatizwa kwa maji mimi huwa ninatoa taarifa kwa umma kwamba nimefanya uamuzi wa kuishi kwa Yesu. Ninaishi maisha mapya. Yesu Kristo sasa anasimamia maisha yangu. Amenipa kusudi jipya maishani. Nguvu zake ndizo zitakazonitia nguvu kila siku. (Tazama pia Warumi 6:4.)

## B. Ni kwa nini nibatizwe kwa maji?

1. Ni njia moja ya kumtii Mungu. Mathayo 28:10-20
2. Ni ushuhuda kwa umma kwamba nimekuwa Mkristo.
3. Ni hatua nyingine katika ukuaji wangu wa kiroho.

## C. Ni wakati gani nanapaswa kubatizwa kwa maji?

Baada ya kuwa Mkristo wa kweli, napaswa kubatizwa kwa maji. (Tazama Matendo 2:38,41; 8:37-38; 19:4-5.) Napaswa kusubiri kwa muda gani? Biblia haituambii unatakiwa kusubiri kwa muda gani baada ya kukubali kuwa Mkristo kabla ya kubatizwa kwa maji. Maandiko yaliyoorodheshwa hapo juu yanaonyesha kwamba watu walibatizwa mara tu baada ya kukubali kuwa Wakristo. Leo makanisa mengi yana madarasa ambayo lazima uhudhurie kabla ya kubatizwa kwa maji.

Walakini, jambo muhimu zaidi la kukumbuka ni kwamba ubatizo wa maji ni ishara ya mabadiliko ambayo tayari yamefanyika katika roho yako. Ubatizo wa maji haukufanyi kuwa Mkristo.

Ikiwa haujatoa maisha yako kwa Kristo, basi wewe si Mkristo. Ikiwa mtu ambaye si Mkristo atabatizwa kwa maji, wao hutumbukia chini ya maji wakiwa watenda dhambi wakavu na kurejea wakiwa watenda dhambi walio lowa maji.

# D. Matokeo ya ubatizo wa maji

Ubatizo wa maji peke yake hautafanya mabadiliko yoyote ya kiroho ndani yako. Ni ushuhuda wa hadharani kwamba umempa Kristo maisha yako. Ni kitendo cha utiifu kwa kile Mungu amekuagiza ufanye.

Je, unapaswa kutarajia nini maishani mwako baada ya kitendo hiki? Tarajia majaribu baada ya kubatizwa kwa maji. Yesu alijaribiwa baada ya kubatizwa kwa maji. Tazama Marko 1:9-13.

Shetani hafurahii kuhusu mabadiliko uliyofanya ya kumkataa kuwa kiongozi wa maisha yako. Atafanya kila awezalo kukukatisha tamaa, ili umkane Mungu. Lakini kumbuka, katika maisha yako mapya katika Kristo, unaahadi kupokea nguvu za Mungu kukusaidia kushinda kila jaribu ambalo Shetani atakuletea maishani mwako.

# Sura ya 6
# Maombi

## A. Maombi ni nini?

### 1. Ufafanuzi

Maombi ni kuzungumza na Mungu. Ni hali ya wewe kuzungumza na Mungu na Mungu anazungumza nawe. Maombi hayapaswi kuwa mazungumzo yanayoyoegemea upande mmoja tu ambapo ni wewe unaongea na Mungu pekee. Mpe Mungu nafasi aongee nawe.

### 2. Ni kwa nini niombe?

Kuna sababu nyingi ni kwa nini unapaswa kuomba kwa Mungu.
Hapa kuna sababu chache.

a. Kupokea msaada kutoka kwa Mungu. (Mathayo 7:7-8)

b. Kuwa na ushirika na Mungu. (Mithali 15:8)

c. Kumwambia Mungu nampenda.

d. Kutii amri ya Mungu ya kuomba.
(1 Wathesalonike 5:17)

e. Kumkaribia Mungu.

f. Kufuata mfano wa Yesu. (Waebrania 5:7)

### 3. Ni kwa nini ninaomba?

Wakati Yesu alikuwa hapa duniani, alimwomba Mungu Baba. Mfano wa Yesu ni mzuri wa kufuata. Hakuna kitu ambacho ni kibaya cha kumwomba Yesu au Roho Mtakatifu.
Ni sawa kuwafikiria wote watatu unapoomba.

Hapa kuna njia moja ya kuelezea mazungumzo yako na hawa watatu wakati unapoomba. Unaomba kwa Mungu Baba, kwa jina la Yesu, kupitia kwa nguvu ya Roho Mtakatifu.

# B. Je, nitaombaje?

## 1. Tumia lugha ya kawaida

Ongea na Mungu kwa njia ile ile ambayo ungeongea na mtu mwingine yeyote. Hakuna maneno maalum ya kutumia wakati wa kuomba. Endelea na mazungumzo na Mungu kama vile ungeongea na rafiki yako.

## 2. Mwambie Mungu ukweli

Unapoomba kwa Mungu, kuwa wewe mwenyewe! Mungu anakujua kuliko mtu mwingine yeyote, kwa hivyo usijaribu kumficha chochote. Fanya maombi yako kuwa wazi na ya kweli kabisa wakati unapozungumza na Mungu. Ikiwa umekasirika, kufadhaika, au umevunjika moyo, mwambie Mungu. Mwambie haswa jinsi unavyohisi na pia mawazo yako.

## 3. Omba jambo maaalum – kwa uhakika

Katika maombi yako, usiombe tu kwa ujumla. Yafanye maombi yako yawe ya kina. Ikiwa utaomba ombi maalum, basi utaweza kushuhudia wakati Mungu anapojibu maombi yako. Sala kama vile, “Mungu awasaidie wote wanaotumia dawa za kulevya ulimwenguni ili wawe Wakristo,” ni maombi ya jumla sana kuwa ya maana.

Walakini, sala ifuatayo ni maalum zaidi. “Mungu, kaka yangu ni mraibu wa dawa za kulevya. Nisaidie wiki hii kuweza kuzungumza naye baadhi ya mambo ambayo Unafanya katika maisha yangu. Nisaidie kumuonyesha upendo kwa njia ambayo atataka kukujua zaidi na kuwa Mkristo.”

## 4. Jinsi mwili wako ulivyokaa sio jambo muhimu

Mkao wa mwili wako si jambo muhimu sana ukilinganisha na jinsi ulivyo makini katika akili na roho yako. Unapoomba, fikiria juu ya kile unachomwambia Mungu. Kuwa katika hali nzuri wakati unaposali. (Lakini hakikisha unakaa macho!)

# C. Napaswa kusema nini ninapoomba?

Unapoomba, unapaswa kumuambia Mungu nini? Huenda ikawa vigumu kwa Wakristo wengine wapya kuomba kwa sababu hawajawahi kuifanya hii kuwa sehemu ya kawaida ya maisha yao ya kila siku. Ni muhimu kuelewa kuwa kuna njia nyingi za kuomba-sio njia moja tu kamili.

Unahitaji kumfikiria Mungu kama rafiki yako, na uongee naye kama vile ungeongea na rafiki yako wa karibu. Hoja zilizoorodheshwa hapa chini ni baadhi ya mambo ambayo unaweza kujumuisha unapozungumza na Mungu. Usijali kuhusu kufanya makosa-yafanye tu! Omba!

## 1. Mwabudu Mungu

Mwambie Mungu kwamba unampenda, na kwamba unamthamini. Kumsifu Mungu ni moja wapo ya njia bora za kumwabudu Mungu. Mojawapo wa njianamna ya kufanya hivyo ni kunukuu maandiko kwa Mungu, kama vile  Zaburi nyingi.

## 2. Muombe Mungu akusamehe dhambi zako

Ikiwa umemwasi Mungu, au umeshindwa kufanya kile unachojua ni sawa, basi mwombe Mungu akusamehe. Tazama Zaburi 66:18 na Isaya 59:2.

## 3. Mshukuru Mungu

Wathesalonike wa Kwanza 5:18 katika tafsiri ya Biblia Takatifu (SUV), inatuambia, “Shukuruni kwa kila jambo, kwa maana haya ndiyo mapenzi ya Mungu kwa ajili yenu katika Kristo Yesu.” Mshukuru Mungu kwa msaada wote ambao amekupa. Mshukuru Mungu kwa yote aliyokufanyia. Mshukuru Mungu kwa kukusaidia kutii Neno Lake. Mshukuru Mungu kwa kukusaidia kutumia kanuni za Biblia katika maisha yako kila siku.

Huenda haitakuwa rahisi, lakini tunahitaji kujifunza kumshukuru Mungu kwa shida anazotuma maishani mwetu. Mshukuru Mungu kwamba atatumia shida hizi kutusaidia kukua. Atatumia shida hizi kutusaidia kujifunza jinsi ya kutegemea nguvu Zake kutusaidia kupitia hali hizi ngumu. Tazama Wafilipi 4:6 na Yakobo 1:2-8.

## 4. Ombea kila kitu

Wafilipi 4:6 katika Tafsiri ya Biblia takatifu (SUV) inasema tujifunze “kuombea kila kitu.” Ombea mahitaji yako na pia ombea mahitaji ya watu wengine. Jifunze njia tofauti za kuzungumza na Mungu kuhusu mambo kadhaa unayokabiliana nayo maishani kila siku. Neno kuu ni “kujifunza.” Inabidi kufanya mazoezi ya kumleta Mungu katika mawazo yetu maishani tunapokabiliana na kila hali kwa siku nzima.

Njia nyingine ya kuomba ni kuangalia maombi yaliyo katika Biblia, na kujiweka kwenye sala hiyo. Fanya hiyo sala iwe yako unapoisoma. Vitabu vingi katika Agano Jipya vilivyoandikwa na Paulo vinajumuisha maombi ndani yavyo - kawaida katika sura ya kwanza. Tazama Waefeso 1:15-23.

## 5. Omba jinsi Roho Mtakatifu anavyokuongoza kuomba

Wakati Yesu alipokuwa akifikia mwisho wa huduma yake hapa duniani, aliwaambia wanafunzi wake kwamba baada ya yeye kuondoka, Roho Mtakatifu atakuja kutusaidia. Wakati mwingine hatujui jinsi ya kuomba juu ya hali fulani. Katika nyakati hizo, tunaweza kumwomba Roho Mtakatifu atusaidie kuomba.

**Waefeso 6:18 Biblia Takatifu (SUV)**

**Mkiomba kwa Roho siku zote katika sala zote na maombi,**
**mkikesha kila wakati mkiwaombea watakatifu wote.**

Biblia pia inatuambia kwamba hata wakati hatujui jinsi ya kuomba kuhusu hali fulani, Roho Mtakatifu atatusaidia jinsi ya kuomba.

**Warumi 8.26 Biblia Takatifu (SUV)**

**Vivyo hivyo, Roho hutusaidia katika udhaifu wetu, kwa sababu hatujui kuomba ipasavyo. Lakini Roho mwenyewe hutuombea kwa uchungu usioweza kutamkwa.**

# D. Faida za kuomba ni zipi?

## 1. Maombi hukusaidia kugundua mambo zaidi kuhusu Baba yako wa Mbinguni

Kwa Wakristo wengine wapya, Mungu huonekana kama mgeni kwao. Kadri unapoomba zaidi, ndivyo unavyozidi kumjua Baba yako wa Mbinguni zaidi. Wakati wanafunzi walipomwuliza Yesu awafundishe kuomba, aliwapa sala rahisi ambayo huanza kwa kuongea na Baba yetu wa Mbinguni.

**Mathayo 6:9 Biblia Takatifu (SUV)**

**Hivi basi, ndivyo iwapasavyo kuomba: " 'Baba yetu uliye mbinguni, Jina lako litukuzwe.**

## 2. Maombi hukusaidia kupata msaada wa Mungu wakati wa shida

Mungu yuko tayari kutusaidia kila wakati. Tunahitaji kujifunza kumwomba Mungu msaada Wake tunapokabiliwa na shida ngumu.

**Waebrania 4:16 Biblia Mtakatifu (SUV)**

**Basi na tukikaribie kiti cha rehema kwa ujasiri, ili tupewe rehema na kupata neema ya kutusaidia wakati wa mahitaji.**

Tazama pia 2 Wakorintho 12:7-10 na Yakobo 1:2-8.

## 3. Maombi hukusaidia kupata amani na utulivu wa Mungu katikati ya shida

Ni rahisi sana kwetu kuwa na wasiwasi au kufadhaika wakati shida zinapotujia maishani. Maombi yanaweza kuwa sehemu yenye nguvu ya kuvunja tabia zetu za zamani na kuwa na jibu la hali hizi ngumu maishani mwetu.

**Wafilipi 4:6-7 Biblia Takatifu (SUV)**

**Msijisumbue kwa jambo lolote, bali katika kila jambo kwa kuomba na kusihi pamoja na kushukuru, haja zenu na zijulikane na Mungu. [7] Nayo amani ya Mungu, inayopita fahamu zote, itailinda mioyo yenu na nia zenu katika Kristo Yesu.**

## 4. Maombi hukusaidia kumpokea Roho Mtakatifu

Baada ya Yesu kurudi mbinguni, wafuasi wa Yesu walikusanyika pamoja kwa maombi kila siku hadi walipopata jibu maalum kutoka kwa Mungu. Roho Mtakatifu alikuja juu yao kwa njia ya pekee na wakazungumza kwa lugha zingine. Tazama Matendo sura ya 2 na Matendo 4:31.

Kwa kila mmoja wetu leo, tuna ahadi kwamba tunapomwalika Yesu mioyoni mwetu, na kumwomba atusamehe dhambi zetu — kwa dakika hiyo hiyo, Roho Mtakatifu anaingia maishani mwetu.

**Luka 11:13 Biblia Takatifu (SUV)**

**“Basi ikiwa ninyi mlio waovu, mnajua kuwapa watoto wenu vitu vizuri, si zaidi sana Baba yenu aliye mbinguni atawapa Roho Mtakatifu wale wamwombao!”**

## 5. Maombi hukusaidia kujua mapenzi ya Mungu kwa maisha yako

Maandiko mengi yanazungumzia mpango wa Mungu kwa maisha yetu. Anataka uelewe mpango Wake juu ya maisha yako. Maombi ni sehemu muhimu sana ya kugundua kile Mungu anataka ufanye. Hata Yesu alimwomba Mungu juu ya kile Mungu alimtaka kufanya.

**Luka 22:41-43 Biblia Takatifu (SUV)**

**Akajitenga nao kama umbali wa kutupa jiwe, akapiga magoti, akaomba**
**42 akisema, “Baba, kama ni mapenzi yako, niondolee kikombe hiki. Lakini si kama nipendavyo, bali mapenzi yako yatendeke.” 43 Malaika kutoka mbinguni akamtokea, akamtia nguvu.**

## 6. Maombi hukusaidia kuwa tayari kwa kurudi kwa Yesu

Yesu alisema anarudi, na kwamba tunapaswa kuwa tayari wakati wote kwa kurudi kwake. Wanafunzi wake walimwuliza Yesu alikuwa anarudi lini, lakini hakuwahi kuwapa tarehe maalum. Badala yake aliwaambia wawe tayari kila wakati. Maombi yanaweza kutusaidia kutilia mkazo siku ya mwisho - ambayo ni muhimu zaidi – hali ya kuwa tayari kwa kuridi kwa Yesu.

**Luka 21:36 Biblia Takatifu (SUV)**

**Kesheni daima na mwombe ili mweze kuokoka na yale yote yatakayotokea na kusimama mbele ya Mwana wa Adamu.**

# E. Ninawezaje kupata majibu ya maombi yangu?

## 1. Tarajia Mungu akujibu

Ikiwa Yesu anatawala maisha yako, na unaombe kwa kulingana na mapenzi yake, basi unaweza kutarajia Mungu akujibu maombi yako. Tazama 1 Yohana 5:14-15. Sisi sote hutaka maombi yetu yajibiwe, lakini Munguhuwa hatupatii kila kitu tunachotaka. Unapoomba, fanya maombi yako yawe wazi ili uweze kujua ikiwa Mungu ameyajibu au la.

Ikiwa hautarajii Mungu kukujibu maombi yako, labda hatayajibu maombi yako. Tazama Yakobo 1:6-7.

## 2. Pokea jibu la Mungu

Wakati mwingine watu hutarajia Mungu kukaa tu mbinguni na kusema "ndio" kila wakati wanapomwomba kitu. Unapomuuliza Mungu kitu, tambua kwamba anaweza kukupatia jibu moja kati ya matatu. Anaweza kusema "Ndio," "Hapana," au "Subiri kidogo." Jibu lolote atakalotoa — likubali.

Paulo aliomba kwa shauku kubwa mara tatu, akimuuliza Mungu aondoe shida maishani mwake. Lakini jibu la Mungu lilikuwa "hapana." Badala yake Mungu alimwambia Paulo atampa nguvu zote anazohitaji kupitia shida hiyo. Tazama 2 Wakorintho 12:7-10. Angalia kwa karibu majibu ya Paulo kwa jibu la Mungu - ingawa jibu lilikuwa "hapana".

# F. Kwa nini sipati majibu ya maombi yangu?

Wengi wetu tunaweza kufikiria nyakati ambazo tumeomba na kumwuliza Mungu kitu, na hatukupata kile tulichoomba. Kama ilivyoelezwa hapo juu, wakati mwingine Mungu hutoa jibu la "Hapana," au "Subiri kidogo." Unahitaji kuelewa kwamba kwa hakika Mungu anataka kuwa karibu nawe. Zaburi 145:18 Tafsiri Biblia Takatifu (SUV) inasema, "Bwana yu karibu na wote wamwitao, karibu na wote wamwitao kwa uaminifu."

Hapa kuna mambo ambayo yanaeleza ni kwa nini hatupati jibu kwa baadhi ya maombi yetu.

## 1. Je, unamwuliza Mungu vitu visivyofaa?

Inawezekana mipango ya Mungu kwako ni tofauti na mipango yako. Wakati mwingine kile tunachotaka sio kile Ametupangia. Ikiwa haupati jibu la maombi yako, basi mwombe Mungu akusaidie kuelewa anachotaka kutoka kwako. Unapomuuliza Mungu swali, ni mara ngapi mbingu imekunyamazia?

**Yakobo 4:14-15 Biblia Takatifu (SUV)**

**Lakini hamjui hata litakalotukia kesho. Maisha yenu ni nini? Ninyi ni ukungu ambao huonekana kwa kitambo kidogo kisha hutoweka. 15 Badala yake, inawapasa kusema, "Kama Bwana akipenda, tutaishi na kufanya hili ama lile."**

**Yakobo 4:3 Biblia Takatifu (SUV)**

**Mnapoomba hampati kwa sababu mnaomba kwa nia mbaya,
ili mpate kuvitumia hivyo mtakavyopata kwa tamaa zenu.**

Wakati mwingine tunamuuliza Mungu kutupatia majibu ambayo yeye hayuko tayari kutupatia. Tunaweza kutaka kujua kitu kuhusu siku zetu za usoni, lakini majibu yake ni - Sitakuambia leo. Mungu mara nyingi hatufunulii maisha yetu ya baadaye — Anataka tujifunze jinsi ya kuishi leo kwa kumtii Yeye. Anajua ni wakati gani mzuri wa kutuambia juu ya siku zetu za usoni. Tunahitaji kujifunza jinsi ya kutumia vyema wakati wetu wa leo.

## 2. Je, umeshikilia dhambi maishani mwako?

Tunaposhikilia dhambi maishani mwetu, tunaweza kuacha maombi yetu wenyewe. Dhambi hututenganisha na Mungu. Hii haimaanishi tunapaswa kuwa wakamilifu kabla Mungu hajajibu maombi yetu. Na mara nyingi Mungu hujibu maombi, hata wakati watu wanaishi katika dhambi. Lakini dhambi inaweza kutuzuia kutoka kwa uhusiano wa wazi na Mungu.

Ikiwa unaona kuwa haupati majibu ya maombi yako, unaweza kuamua kusema, “Mungu ikiwa kuna dhambi maishani mwangu ambayo inanizuia kusikia majibu yako kutokana na maombi yangu, tafadhali nisaidie kuiona ni dhambi gani hiyo.
Ninataka kukiri, na kusogea karibu na wewe.”

**Zaburi 66:18 BibliaTtakatifu (SUV)**

**Kama ningekuwa nimeyaficha maovu moyoni mwangu,
Bwana asingekuwa amenisikiliza;**

**Mithali 28:13 Biblia Takatifu (SUV)**

**Yeye afichaye dhambi zake hatafanikiwa, bali yeyote aziungamaye
na kuziacha hupata rehema**

## 3. Je, unakataa kumsikiliza Mungu?

Ikiwa uko tayari kusikia “Ndio” kutoka kwa Mungu kila wakati unapoomba, basi usishangae wakati ambapo maombi yako hayajibiwi. Tunahitaji kuwa na mtazamo wa- “Mungu nataka kusikia kutoka Kwako. Niambie chochote unachotaka, kwa sababu ninataka kukutii.”

**Mithali 28:9 Biblia Takatifu (SUV)**

**Kama mtu yeyote akikataa kusikia sheria, hata maombi yake ni chukizo.**

## 4. Maombi mengine yana masharti

Maombi mengine hayatajibiwa mpaka kwanza tufanye kile Mungu anataka tufanye. Utiifu mara nyingi ni sharti la kupata jibu kutoka kwa Mungu. Hatuwezi kusema, “Mungu, niambie kile ninachotaka kusikia, ndipo nitakutii.” Badala yake, tunahitaji kusema, “Mungu, niko tayari kukutii leo, na nitakutii hatua moja kwa wakati, hata ikiwa sitasikia jibu maalum kutoka Kwako.”

Hapa kuna baadhi ya masharti abayo yanaweza kuathiri maombi yetu.

1. Lazima ukiri dhambi zako.
2. Lazima uwe na dhamiri safi.
3. Lazima uonyeshe upendo kwa wengine kila wakati. (1 Wakorintho 13)
4. Lazima usamehe wengine ambao wanaweza kuwa wamekuumiza.

**1 Yohana 3:22-24 (Tafsiri ya Biblia Takatifu SUV)**

**Nasi tutapokea kutoka kwake chochote tuombacho kwa sababu tunamtii na tunafanya mambo yanayompendeza.**

**[23] Na hii ndiyo amri yake: Lazima tuamini katika jina la Mwanawe, Yesu Kristo, na kupendana, kama vile alivyotuamuru. [24] Wale wanaotii amri za Mungu hukaa katika ushirika naye, na yeye naye. Na tunajua anaishi ndani yetu kwa sababu Roho aliyetupa huishi ndani yetu.**

### 5. Je, unaishi kwa shaka?

Wakati mwingine shaka na kutokuamini kunaweza kuzuia maombi yetu kujibiwa. Ikiwa hauamini Mungu atajibu maombi yako, basi shaka lako linaweza kuwa ndicho kitu kinachosimamisha jibu lako kutoka kwa Mungu.

**Waebrania 11:6 Biblia Takatifu (SUV)**

**Lakini pasipo imani haiwezekani kumpendeza Mungu, kwa maana yeyote anayemjia Mungu lazima aamini kwamba yeye yuko na ya kuwa huwapa thawabu wale wamtafutao kwa bidii.**

**Yakobo 1:6-7 Biblia Takatifu (SUV)**

**Lakini anapoomba, lazima aamini wala asiwe na shaka, kwa sababu mtu aliye na shaka ni kama wimbi la bahari, lililochukuliwa na upepo na kutupwa huku na huku. [7] Mtu kama huyo asidhani ya kuwa atapata kitu chochote kutoka kwa Bwana.**

Lakini unapomwuliza, hakikisha kuwa unatarajia ajibu, kwani akili yenye mashaka haijatulia kama wimbi la bahari ambalo linaongozwa na kutupwa na upepo.
Watu kama hao hawapaswi kutarajia kupokea chochote kutoka kwa Bwana.

## G. Ninaomba lini?

### 1. Kamwe usiache kuomba

1 Wathesalonike 5:17 katika Biblia Takatifu (SUV) inasema, “Ombeni bila kukoma.”
Hii inamaanisha kuwa unapswa kujua kuwa Mungu anasikiliza kila wakati.
Kumbuka unaweza kuendelea na mazungumzo naye wakati wowote.
Unapaswa kuwa na tabia ya sala kila wakati.

### 2. Kuwa na wakati wa uliotulia wa kuomba kila mara

Jaribu kupanga wakati wa kawaida kila siku ambapo unaweza kuwa peke yako kwa dakika chache kuomba. Tazama Mathayo 6:6.

### 3. Maombi ya kikundi

Kuna fursa nyingi za kuomba pamoja na watu wengine - huduma za kanisa, makanisa, vikundi vidogo, mikutano ya familia, n.k.

## H. Ni kwa nini maombi ni magumu?

Usishangae ikiwa unapata shida kuomba. Ikiwa haujawahi kuomba sana hapo awali, basi unaweza kuhangaika. Hakuna ufunguo wa kimiujiza wa kufanya maombi kuwa jambo rahisi katika maisha yako yote. Lakini unapoendelea kuomba, utajifunza jinsi ya kuifanya maombi yawe sehemu muhimu zaidi kila siku.

### 1. Je, umemkasirikia Mungu?

Kwa sababu ya uzito na machungu mengi ya zamani, mara nyingi Wakristo wanapambana na swala la kuwa na hasira dhidi ya Mungu. “Ikiwa Mungu ananipenda kweli, kwa nini aliruhusu dhuluma hii sasa?” Au labda hasira ni kwa sababu haupati majibu kutoka kwa Mungu.

Wakati watu wengine walio karibu nawe wanamkasirikia Mungu, hiyo pia inaweza kutikisa imani yako kwa Mungu. Usiruhusu shida za watu wengine zikunyang'anye ukaribu wako na Mungu. Tazama Ayubu 21:15.

### 2. Je, unauhakika kwamba Mungu anasikia maombi yako?

Kuomba kunaweza kuwa jambo gumu kwa Wakristo wapya. Unaweza kuuliza, “Ninaweza kujuaje kwamba Mungu anasikiliza kweli? Inaonekana kama ninajizungumzia”.

Unahitaji kuwa mwangalifu kuangalia msingi wa maombi yako kwa yale ambayo Biblia inasema, sio jinsi akili au mawazo yako yanavyokuambia. Biblia inatuambia tuombe.

**Marko 11:24 Biblia takatifu (SUV)**

**Kwa sababu hiyo nawaambia, yoyote mtakayoyaomba mkisali, aminini ya kwamba mmeyapokea, nayo yatakuwa yenu.**

Hakikisha “unaamini” katika mambo yanayowiana na mapenzi ya Mungu. Kuwa na imani kwa kile ninachotaka sio dawa ya moja kwa moja ya kujibiwa maombi yangu.

## 3. Je, unakabiliwa na shida nyingi katika maisha yako?

Ingawa kuomba siku ya Jumapili kanisani kunaweza kuwa rahisi, ombi linaweza kuwa gumu sana haswa ikiwa unapambana na vishawishi vikubwa, shinikizo za nyumbani, shinikizo kutoka kazini, au shuleni. Ikiwa shida hizi zote zinaendelea kunizidi nguvu, kwa nini niombe?

Wakati shida zinakuzunguka kwa kila upande, basi unapaswa kuyafanya maombi kuwa nafasi kubwa kwa maisha yako ya kula siku-hata ingawa mambo hayatakuwa mazuri.

**Luka 18:1 Biblia Takatifu (SUV)**

**Kisha Yesu akawapa wanafunzi wake mfano ili kuwaonyesha kuwa yawapasa kuomba pasipo kukata tamaa.**

**Yakobo 5:13 Biblia Takatifu (SUV)**

**Je, mtu yeyote miongoni mwenu amepatwa na taabu? Basi inampasa aombe. Je, kuna yeyote mwenye furaha? Basi na aimbe nyimbo za kusifu.**

## 4. Je, unakabiliwa na mateso?

Unapoishi na mtu mgumu, au unakabiliwa na mateso kutoka kwa wengine, je, wewe humwambia Mungu nini? Je, maombi yako ni; Mungu, niondoe hapa! Au kumtoa mtu huyu kutoka kwa maisha yangu!

Yesu alikuwa na ushauri mahususi kabisa wa kutupatia juu ya jinsi tunavyoweza kuomba wakati watu wanafanya maisha kuwa magumu kwetu.

**Mathayo 5:44 Biblia Takatifu (SUV)**

**Lakini ninawaambia:Wapendeni adui zenu na waombeeni wanaowatesa ninyi.**

Unapotafuta kumfanya Mungu awe sehemu muhimu zaidi ya maisha yako, atakusaidia. Atakupatia nguvu na hekima na upendo kwa kila hali unayokabiliana nayo.
Endelea tu kuzungumza naye—kila siku!

Kwa kusoma na kujifunza zaidi, tafadhali tembelea tovuti yetu katika www.iteenchallenge.org.